

HALI YA WILAYA YA KARAGWE

TAARIFA FUPI YA WILAYA YA KARAGWE KWA MHESHIMIWA WILLIAM OLE NASHA (MB), NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI KATIKA ZIARA YAKE WILAYANI KARAGWE

TAREHE 05/06/2017

1.0 UTANGULIZI:

Mh. Naibu Waziri,

Awali ya yote kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Karagwe nichukue fursa hii kukukaribisha katika wilaya yetu wewe na msafara wako. Aidha nikupongeze wewe binafsi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Uteuzi huu unaonyesha ni jinsi gani Mheshimiwa Rais alivyo na imani kwako katika kuongoza Wizara hii. Hongera sana.

2.0 HALI YA ULINZI NA USALAMA

Mh. Naibu Waziri,

Hali ya Ulinzi na Usalama katika Wilaya yetu ni shwari, Mipaka yetu yote ipo Salama

3.0 SEKTA YA MIFUGO

Mh. Naibu Waziri,

Sekta ya mifugo katika wilaya ya Karagwe inachangia pato la Wilaya kwa asilimia 10. Wakazi wa Wilaya ya Karagwe hutegemea mifugo kama chanzo chao cha mapato. Wilaya inayo jumla ya ng'ombe wa asili wapatao 87,610 na ng'ombe wa kisasa 4,324, mbuzi 94,475, Kondoo 4,780 ambapo eneo lililopo kwa ajili ya malisho ni hecta 154,000 tu.

Pia uzalishaji wa maziwa ni mkubwa ambapo lita 64,875,205 uzalishwa kwa mwaka

3.1 Maeneo maalum yaliotengwa kwa ajili ya Wafugaji

Mhe Naibu Waziri

Wilaya ya Karagwe imetenga maeneo ya shughuli za ufugaji kama jedwali linavyoonyesha hapa chini

3.1 JEDWARI LA MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA WAFUGAJI

S/N	MKOA	HALMASHAURI	KATA	KIJIJI	MAENEO YANAYOTUMIKA HADI SASA	
					LINATUMIKA	MAELEZO
1	KAGERA	KARAGWE	Chanika	Kahundwe	V	
2	KAGERA	KARAGWE	Nyakahanga	Kashanda	V	Kuna uvamizi wa wakulima kesi ipo mahakamani
3	KAGERA	KARAGWE	Katanda	Katanda	V	Ni eneo

						lililotolewa na serikali kutoka kwenye vitaru vya Kitengure hecta 2000
4	KAGERA	KARAGWE	Nyakasimbi	Nyakalilo	V	
5	KAGERA	KARAGWE	Nyakahanga	Kakashombwa	V	Kuna uvamizi wa wakulima
6	KAGERA	KARAGWE	Rugu	Ruhita Chenjuba	V	Kuna uvamizi wa wakulima
7	KAGERA	KARAGWE	Nyakakika	Ngembe	V	Maeneo haya yamevamiwa na wakulima
8	KAGERA	KARAGWE	Nyakakika	Kanywamagana	V	Maeneo haya yamevamiwa na wakulima

Licha ya kutengwa kwa maeneo hayo kama jedwali linavyoonyesha hapo juu ,kumekuwa kukijitokeza migogoro kati ya wakulima na mafugaji iliyopelekea maeneo kadhaa kufikishana mahakamani mfano kijiji cha kashanda,Kijiji hiki kilitengwa kisheria mwaka..... kwa ajili ya shughuli za wafugaji tu lakini wakulima wamekuwa waking'ang'ania kukitumia kwa shughuli za kilimo,Mwaka 2015 kamati ya ulinzi na Usalama ya Wilaya ili amru wakulima wote waliovamia kijiji hicho kuondoka lakini wakulima hao walikimbilia mahakamani kuweka zuio la wao kuondolewa katika eneo hilo,,hata hivyo kesi imechukua muda mrefu sana matokeo yake kumeendelea kutokea migogoro ya mara kwa mara.

.Aidha kijiji cha kahundwe Wakulima walifungua kesi mahakamani ya kudai eneo hilo litumike kwa shughuli za kilimo lakini Wafugaji walishinda kesi hiyo,pamoja na wafugaji kushinda kesi bado wakulima wanang'ang'ania maeneo hilo.

Licha ya kuwepo maeneo yalitotengwa kwa ajili ya shughuli za ufugaji bado Wilaya inayo changamoto ya mifugo iliyoko katika vijiji ambavyo vina mchanganyiko wa shughuli za kilimo na ufugaji, hali inayopelekea uwepo wa migogoro ya mara kwa mara juu ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji .

Ilikukabiliana na changamoto hizo wilaya imeisha toa maelekezo kwa ungozi wa serikali za vijiji kutenga maeneo ya shughuli za kilimo na ufugaji.Aidha Wilaya pia imekuwa ikichukua hatua za dharura kusuruhisha migogoro inapotokea,Mfano migogoro iliyojitokeza katika vijiji vya kashanda ,Kahundwe ,Chabuhola, Kanogo ,Bweranyange Nyakasimbi,Mshabaigulu na Katanda.

Mh Naibu Waziri

Licha ya kuwepo kwa migogoro hiyo kwa sasa hakuna migogoro ambayo imepelekea kupoteza maisha ya watu, hii ni kutokana na juhudi kubwa zinazo fanywa na kamati ya Ulinzi na Usalama za kuchukua hatua za mapema pale inapobainika kuwepo kwa migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji.

Mhe Naibu waziri

Sekita hii ya mifugo pia inakabiliana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wake wa majukumu ya kila siku ambayo ni

1.Kuwepo kwa mifugo mingi inayoingizwa kwa njia haramu kutoka nchi jirani za Rwanda na Uganda inayochangia kuwepo kwa migogoro ardhi ya mara kwa mara pamoja na milipuko ya magonjwa ya mifugo.

2. Upungufu wa eneo la malisho kulingana na idadi ya mifugo iliyopo kwa sasa kwani Wilaya kwa sasa ina jumla ya hecta 154,000 inayotosha idadi ya mifugo 61,600 tu.
3. Ukosefu wa Viwanda vidogo vidogo/vituo vya kukusanyia maziwa

Mh, Naibu Waziri,

Kulingana na changamoto zilizopo tunaomba kupitia Wizara yako utusaidie yafuatayo;

- i. Kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza kwa kujenga viwanda vya maziwa ili thamani ya maziwa ipande na kuongeza pato la Taifa na mfugaji
- ii. Kwa kuwa Wilaya yetu ipo mpakani na imezungukwa na hifadhi za akiba tunaomba serikali itupatie chanjo za mifugo kwa bei nafuu ili kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ambayo yanasababisha vifo kwa mifugo
- iii. Kuongezewa Maafisa ugani wa mifugo/uvuvi na daktari wa mifugo

HITIMISHO

Mh. Naibu Waziri,

Tunapenda kuhitimisha taarifa hii, kwa kukutaarifa kuwa kwa sasa Wilaya yetu haina upungufu wa chakula wilaya inacho chakula cha kutosha katika msimu huu. Aidha tunapenda kukushikru kwa mara nyingine tena kwa kutenga muda wako kuja kutembelea Wilaya yetu tunakutakia afya njema siku zote katika utekelezaji wako wa majukumu ya kila siku.

Geofrey A. Mheluka
MKUU WA WILAYA
KARAGWE